

ANZA KUFUGA KUKU Kimkakati

Jipatie Pesa za ziada na lishe bora



99%
FANIKIWA KIKWELI

Je wajua?
Tetea 10 + miezi 6=400 kuku

MAKINIKA

**XAVERY
DANKAN**

No 1

UTANGULIZI

Huenda unajiuliza maswali haya;

Je, ninaweza kupata kipato chenye tija kupitia ufugaji wa kuku?

Jibu ni ndio.

Fikiria una kuku 100 na unauza kwa bei ya jumla Tsh 10,000/= utakuwa na milioni 1 ya pamoja. Hivyo ukiwa na mradi unaotoa kuku 100 kila mwezi basi unaweza kuwa na kipato cha million 1 kila mwezi. Je, hujapata kipato chenye tija?

Je, ninaweza kuboresha lishe katika familia yangu kupitia ufugaji wa kuku?

Bila shaka!

Kupitia mayai ya kuku au nyama yake, unaweza kupata protini iliyo bora na inayopendekezwa zaidi na madaktari kwani kuku hutoa nyama nyeupe iliyo bora zaidi kiafya. Vilevile samadi ya kuku ni yenye ubora sana kwani inamadini muhimu yahitajikayo katika mimea, hivyo unaweza kuitumia kukuza mbogamboga na hivyo kuboresha upatikanaji chakula bora katika familia.

Ninawezaje kufanikiwa katika ufugaji bora wa kuku?

Huenda ukajiuliza hili labda umejaribu kufuga lakini changamoto zimekuangusha. Huenda umeona fulani akifanikiwa katika ufugaji wa kuku nawe umetamani kufuga lakini hujui jinsi ya kuanza.

Habari njema ni kwamba kitabu hiki kitakuongoza ama kukupa maarifa bora ambayo ukichanganya na ujuzi wako utakuwa mfugaji bora zaidi na mwenye mafanikio wa kuku wa kienyeji na hata wa kisasa kwani kimeandikwa kupitia ujuzi na uzoefu niliokusanya kwa miaka mitano katika utafiti wa kufuga kuku kibinafsi na kwa kujifunza kutoka kwa wengine.

Uandaaji wa kitabu hiki, umetegemea utafiti wa kina katika maeneo yaliyoko kusini magharibi mwa Tanzania. Hivyo mfugaji wa maeneo hayo anaweza kunufaika zaidi japo kinaweza kuifaa nchi nzima.

Picha zilizotumika ni kutoka vyanzo vya kimtandao kupitia tovuti mbalimbali za kiufugaji.

SHUKRANI

Shukrani zangu za kwanza zimwendee Muumba wa mbingu na nchi kwa kunitunza na kunibariki katika utulivu wa kuandaa kijitabu hiki richa ya magumu.

Shukrani za pili ni kwako msomaji, ambaye umetumia wakati wako na jitihada ili kujipatia kitabu hiki.

simulizistar

YALIYOMO.....

Sura ya kwanza..... pg 1.

Dondoo za ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Sura ya pili pg 13.

Banda bora la kuku.

Sura ya tatu..... pg 21.

Jinsi ya kukuza au kulea vifaranga.

Sura ya nne..... pg 26.

Magonjwa hatari kwa Kuku

Sura ya tano..... pg 33.

dondoo za biosecurity na tiba kiujumla

Sura ya sita..... pg 36.

kutunza kumbukumbu za mradi

Sura ya saba..... pg 41.

masoko.

Sura ya nane..... pg 42.

Siri 6 za kuwa na kuku 400 na kuendelea wa kienyeji kwa miezi

simulizistar

sita tu.